

MWONGOZO WA KIDATO CHA KWANZA

Ufahamu

- a) Elimu humfaidi mtu kwa njia kama vile kiuchumi, kisayansi, kiutafiti-ndio msingi wa maendeleo ya maarifa 1x2
- b) Mawasiliano duni
Matumizi duni ya maliasili
Ukosefu wa maarifa ya kujipatia vyakula
Kutonufaika kutoekana na maandishi
Kutofaidi uhondo wa Sanaa ya uandishi/fasihi na mafunzo yake $4 \times 1 = 4$
- c) Kujua kusoma na kuandika ili kurahisisha Maisha kwa kutegemea ujuzi huo kukabili na kutatua matatizo maishani
- d) Mawasiliano ni uwezo wa kupashana au kupochezana ujumbe- $1 \times 1 = 1$
Mifano: simu, barua, telegram, mazungumzo ya ana kwa ana $2 \times 1 = 2$
- e) Methali inaashiria jinsi mtu asiyejua mambo anavyoweza kubabaishwa hata na mambo madogo ilhali mjuzi anayaelewa na kuyamudu bila wasiwasi. $1 \times 2 = 2$
- f) Madini-mawe ya thamani
Ombwe-kitu kitupu 1x2=2

Matumizi ya lugha

- a) /w/-mdomo
/d/-ufizi 1x2=2
- b) Katika utamkaji wa irabu, hewa haizuiliwi mahali popote, ilhali katika utamkaji wa konsonanti hewa huzuiliwa kwenye ala mbalimbali za kutamkia. $2 \times 2 = 4$
- c) Vipasuo-/p/, /b/, /t/, /d/, /j/, /k/, /g/
Kipasuo-kwamizo-/ch/
Vikwamizo-f,v,th,dh,s,z,sh,gh,h
Nazali-m,n,ny,ng'

MWONGOZO WA SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

- Kimadende-r
Nusu irabu-w,y
Kitambaza-l $1 \times 7 = 7$
- d) Anako-chez-ea.
Awali tamati $1 \times 2 = 2$
- e) Sauti-silabi-neno-sentensi nusu kwa kila kipashio=2
- f) Shadda-ni mkazo kwenye silabi Fulani ya neno ili kuleta maana halisi
Kiimbo-mawimbi ya sauti yanayopanda na kushuka mtu anapozungumza
 $2 \times 2 = 4$
- g) Mwamba $1 \times 2 = 2$
- h) Marudi'o, karata'si 1
- i) Viambishi-viungo vyenye maana ya kisarufi ambavyo huambatishwa kwenye mzizi wa neno ili kulipa neno hilo maana.
Kihisishi-ni neno linalotoa hisia za moyoni
Kiwakilishi-huchukua nafasi ya nomino $3 \times 1 = 3$
- j) Nelson Mandela, aliyekuwa Rais wa Afrika Kusini, alifanya mashauri na Mobutu Sesseko wa Zaire. Alama 2
- k) Mpwa wangu atafua nguo zake. $1 \times 2 = 2$
- l) Mama anapakua ilhali dada anaanua nguo. $1 \times 2 = 2$
- m) Kina baba wanachimba visima $1 \times 2 = 2$

ISIMUJAMII

Majukumu ya lugha

- i. Kitambulisho cha jamii
- ii. Hutumika kuwasiliana
- iii. Hutumika kufahamishana/kupashana habri
- iv. Hutumika kupatanisha na kuleta umoja katika jamii
- v. Hutumika katika kuliwaza

MWONGOZO WA SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

- vi. Hutumika katika kuonya
- vii. Husaidia binadamu kuyaolewa mazingira yake
- viii. Lugha ni chombo cha kimsingi katika kuendeleza taaluma za aina nyingi kama vile elimu, sheria, teknolojia, michezo n.k $10 \times 1 = 10$

Dhima ya fasihi

- i. Ni kitambulisho cha jamii
- ii. Hupumzisha/huburudisha/huliwaza
- iii. Huhifadhi na kurithisha maarifa au elimu ya jamii
- iv. Hukuza lugha
- v. Humwezesha binadamu kujenga tabia ya kudadisi na kutafakari kuhusu masuala yanayomkumba
- vi. Huhamasisha wanajamii kuhusu maswala ibuka na nyeti katika jamii
- vii. Huhifadhi historia ya jamii
- viii. Hupumbaza kwa kuathiri hisia za binadamu.

Tofauti kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi

Fasihi simulizi	fasihi andishi
i. Huwasilishwa kwa njia ya mdomo	kwa maandishi
ii. Huhifadhiwa akilini	kwa maandishi
iii. Hubadilishwa papo kwa hapo jukwaani	hayabadiliki ila kwa kuandikwa tena
iv. Ni mali ya jamii	mali ya mwandishi
v. Muundo rahisi kufuatika	huwa changamano
vi. Uzuri wake hutegemea wasilisho jukwaani	hutegemea usanii wa mwandishi
vii. Sifa zake za zamani hupotea	hudumu kwa muda mrefu
viii. Hadhira huweza kuathiri uwasilishaji moja	hadhira haina mchango wa moja kwa moja

MWONGOZO WA SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

Zozote $5 \times 2 = 10$